# KAMISHENI YA KUSIMAMIA NGUMI ZA KULIPWA

# TANZANIA

# PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION

# (TPBRC)

## KANUNI, TARATIBU NA SHERIA ZA MSINGI ZINAZOONGOZA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA TANZANIA

***(Kama zilivyothibitishwa 2019. Marekebisho ya Septemba 8, 2022).***

TOLEO LA MWAKA 2022

UTANGULIZI

Kanuni hizi ***Kama zilivyothibitishwa 2019. Marekebisho ya Septemba 8, 2022*** zinahusisha sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji wa mchezo wa ngumi za kulipwa zenye lengo pia la kulinda afya na maslahi ya bondia, maslahi ya waandaaji katika kuleta maendeleo na ukuzaji pamoja na kuuweka karibu mchezo wa ngumi za kulipwa kwa jamii. Hivyo basi, Kamisheni itazitumia Kanuni hizi katika kuendesha mchezo wa ngumi za kulipwa Tanzania. Vilevile, Kanuni hizi ndizo zitakazotumika katika kuongoza mapambano yote ya ngumi za kulipwa ambayo yatasimamiwa na Kamisheni.

## 1.0. SHERIA NA KANUNI ZA VYAMA SHIRIKISHI ZINAZOONGOZA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA

Ili kutenda haki, kulinda afya, hadhi na maslahi miongoni mwa wadau wote wa ngumi za kulipwa, kwa mapambano ya ubingwa wa kimataifa, utekelezaji wa sheria na taratibu zote zitakazofuatwa ni za chama husika ambazo zitasomwa na kufafanuliwa kwa mabondia na maofisa wa mchezo husika katika kikao cha pamoja kati ya mabondia maofisa wa mchezo huo pamoja wawakilishi wa chama hicho na viongozi wa Kamisheni .

Katika Maktaba yake, Kamisheni itakuwa na nakala amilifu ya Sheria na Kanuni za Vyama vyote vya kimataifa vya masumbwi vinavyotambulika duniani.

## 2.0. BONDIA WA NGUMI ZA KULIPWA

Kulingana na sheria na taratibu za kimataifa za mtu kutambulika kama bondia wa kulipwa; mtu yeyote nchini Tanzania, atatambulika kama bondia wa kulipwa endapo atakuwa ametimiza vigezo na masharti yote yafuatayo: -

2.1. Awe ametimiza umri wa zaidi ya miaka kumi na saba (17) wakati anajiunga katika mchezo wa ngumi za kulipwa na atalazimika kuwa leseni ya ngumi za kulipwa kabla hajaanza kupanda ulingoni. Ili kudhibitisha umri wake, bondia atawajibika kuwasilisha nakala halisi ya kitambulisho chochote

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

kinachotolewa na serikali kama vile; kadi ya mpiga kura, leseni ya kuendesha vyombo vya moto, kitambulisho cha NIDA, hati ya kusafiria, n.k.

2.2. Ni muhimu awe amecheza mizunguko isiyoungua hamsini (50) kwenye ngumi za wazi

2.3. Iwapo ataanzia moja kwa moja katika ngumi za kulipwa atalazimika kucheza mapambano ya mizunguko minne (4) yasiyopungua sita (6) yenye mizunguko isiyopungua ishirini na nne (24) na mapambano ya mizunguko sita (6) yasiyopungua manne (4) yenye jumla ya mizunguko ishirini na nne (24).

Kamati ya Ufundi ya Kamisheni inaweza kuruhusu bondia ambaye ataonesha umahiri na ustadi, kushiriki mapambano ya mizunguko zaidi kabla ya kukamilisha mizunguko iliyotajwa hapo endapo tu itajiridhisha na uwezo wa bondia huyo.

2.4. Bondia aliyecheza mizunguko kama ilivyoelekezwa katika aya ya 2.3. hapo juu anaruhusiwa kushiriki katika mapambano ya mtoano (elimination) ya kuwania ubingwa wa taifa,

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

## 3.0. MADARAJA YA UZITO (WEIGHT DIVISIONS) YANAYOTAMBULIKA KATIKA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA.

### 3.1. Madaraja ya uzito

Uzito na madaraja ya uzito kwa mabondia wa kulipwa ambavyo vinatambulika katika Kamisheni ni viwango vya kimataifa vinavyokubaliwa na vyama vyote vya ngumi za kulipwa duniani. **NI LAZIMA** bondia afikie viwango vya uzito katika madaraja yaliyotajwa kama ilivyoorodheshwa katika jedwali la uzito hapa chini: -

| DARAJA | PAUNDI | USIOZIDI KILOGRAMU |
|---|---:|---:|
| Strawweight | 105 | 47.627 |
| Jr. Flyweight | 108 | 48.988 |
| Flyweight | 112 | 50.802 |
| Super Flyweight/ Jr. Bantamweight | 115 | 52.163 |
| Bantamweight | 118 | 53.525 |
| Super Bantamweight | 122 | 55.225 |
| Featherweight | 126 | 57.153 |
| Super Featherweight/Jr. Lightweight | 130 | 58.967 |
| Lightweight | 135 | 61.235 |
| Super Lightweight/Jr. Welterweight | 140 | 63.503 |
| Welterweight | 147 | 66.678 |
| Super Welterweight/Jr. Middleweight | 154 | 69.853 |
| Middleweight | 160 | 72.574 |
| Super Middleweight | 168 | 76.203 |
| Light Heavyweight | 175 | 79.378 |
| Cruiserweight | 190 | 86.183 |
| Heavy Weight | 200+ | 90.892 |

3.1.1. M t u y e y o t e a n a y

3.2. Bondia hatoruhusiwa kupigana endapo atazidi ukomo wa uzito kwa madaraja kama ifuatavyo: -

| Na. | Uzito (paundi) | Uzito (Kg) | Uzito (paundi) | Uzito (Kg) |
|---|---|---|---|---|
| | Uzito | | Ukomo | |
| 1. | 118 | 53.552 | 3 | 1.389 |
| 2. | 118 – 130 | 53.552 – 58.995 | 4 | 1.843 |
| 3. | 130 – 140 | 58.995 – 63.531 | 5 | 2.296 |
| 4. | 140 – 175 | 63.531 – 79.407 | 7 | 3.203 |
| 5. | 175 – 190 | 79.407 – 86.211 | 9 | 4.111 |
| 6. | 190 – 200 | 86.211 – 90.747 | 12 | 5.471 |
| 7. | 200+ | 90.747+ | Haina ukomo | |

## 4.0. TARATIBU ZA UPIMAJI AFYA NA UZITO KWA MABONDIA NA MAOFISA

### 4.1. UPIMAJI AFYA

4.1.1. Kabla ya kushiriki pambano lolote la ngumi za kulipwa bondia atawajibika kupimwa afya yake na daktari anayetambulika na chama cha madaktari wa tiba za michezo (TASMA) na mwenye leseni

ya udaktari, mara baada ya vipimo, daktari atashauri iwapo bondia husika anaweza au hawezi kushiriki pambano.

4.1.2. Kamisheni itazingatia ushauri wa daktari kuhusu hali ya afya na uwezo wa bondia husika kiafya katika kushiriki pambano na **HAITARUHUSU** pambano kufanyika iwapo daktari atashauri bondia husika asicheze katika pambano hilo kutokana na sababu za kiafya.

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

4.1.3. Bondia ambaye atapigwa kwa KO ama TKO atalazimika kupimwa tena afya ndani ya masaa ishirini na nne (24 hours) katika hospitali ya serikali mara baada pambano husika kumalizika na

atawajibika kuwasilisha matokeo ya vipimo hivyo katika Kamisheni.

4.1.4. Bondia atakayeshindwa pambano kwa kanuni ya TKO au KO atasimamishwa kushiriki mapambano ya ngumi za kulipwa kwa kwa muda ambao daktari atashauri baada ya kumpima punde tu mara baada ya kushuka ulingoni..

4.1.5. Bondia yeyote atakayefanya udanganyifu wa kupelekea kupoteza pambano ulingoni kwa pambano litakalofanyika Tanzania, atafungiwa kutocheza ngumi kwa miezi ishirini na nne (24) na atakatwa asilimia hamsini (50%) ya malipo yake kwa mujibu wa mkataba na fedha hizo kuwekwa katia mfuko wa Kamisheni.

4.1.6. Bondia wa Tanzania atakayefanya udanganyifu wa kupelekea kupoteza pambano ulingoni kwa pambano litakalofanyika nje ya Tanzania, atafungiwa kutocheza ngumi kwa miezi ishirini na nne (24) na atakatwa asilimia hamsini (50%) ya malipo yake kwa mujibu wa mkataba na fedha hizo kuwekwa katia mfuko wa Kamisheni.

4.1.7. Kila anapohuisha leseni yake, bondia au ofisa wa ulingoni atawajibika pia kupima afya na kuwasilisha matokeo ya vipimo vya afya yake kama itakavyoelekezwa na Kamisheni.

## 4.2. KUPIMA UZITO

4.2.1. Kamisheni itamteua msimamizi katika zoezi la kupima uzito. Msimamizi huyo atawajibika kuhakikisha kwamba mzani utakaotumika kupimia uzito ni mzani uliohakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.

4.2.2. Mabondia, maofisa pamoja na msimamizi wa zoezi la upimaji uzito watawajibika kuwepo katika eneo lililopangwa kwa zoezi la kupima uzito angalau masaa mawili kabla ya zoezi hilo kuanza.

4.2.3. Mabondia wote wanaopigana, WATALAZIMIKA: -

4.2.3.1. kupima uzito mdani ya masaa ishirini na nne (24) au kumi na mbili (12) kabla ya pambano husika,

4.2.3.2. Muandaaji atawajibika kuhakikisha mzani utakaotumika rasmi kupimia uzito unakuwepo katika eneo lililopangwa kwa zoezi hilo angalau saa moja kabla zoezi la kupima uzito kuanza rasmi kwa muda uliopangwa ili kuwapa fursa mabondia kubaini uzito wao kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi la upimaji uzito,

4.2.3.3. Kwa mapambano ya Kimataifa,

4.2.3.3.1. bondia kutoka nje ya Tanzania atawajibika kuwasilisha kwa msimamizi wa zoezi la kupima uzito nakala halisi ya ruhusa ya kucheza nje ya nchi (clearence) iliyotolewa na mamlaka inayohusika na kusimamia ngumi za kulipwa nchini mwake kabla ya kuanza kwa zoezi la kupima uzito na afya,

4.2.3.3.2. Muandaaji atawajibika kuwasilisha nakala ya mkataba wa pambano kati yake na bondia kutoka nje pamoja na taarifa ya matokeo ya vipimo vya afya kwa Kamisheni siku ishirini (20) kabla ya pambano na

atawasilisha nakala halisi za nyaraka hizo kabla ya zoezi la kupima uzito na afya halijafanyika.

4.2.4. Katika zoezi la upimaji uzito, mabondia watavaa nguo zenye kusitiri maungo yao na kuthibitishwa na msimamizi wa zoezi hilo kabla hawajapanda kwenye mzani.

4.2.5. Matokeo ya zoezi la upimaji uzito kwa mabondia ndiyo yatakayobainisha daraja la uzito kwa bondia husika na aidha kuendelea au kutoendelea kwa pambano pamoja na taratibu nyingine kama inavyobainishwa katika aya zinazofuata hapa chini: -

4.2.5.1. Endapo bondia atakutwa na uzito zaidi ya anaopaswa kuwa nao kwa mujibu wa mkataba wa pambano wakati wa zoezi la upimaji uzito, atapewa muda wa masaa mawili (2) ili aweze kupunguza uzito huo na kufikia kiwango kinachostahili. Endapo bondia aliyezidi uzito atashindwa kupunguza uzito katika muda huo, hatoruhusiwa kucheza pambano husika.

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION TPBRC P.O. Box No. 9968, Dar Es Salaam

4.2.5.2. Endapo, kwa sababu yoyote ile, zoezi la kupima uzito litafanyika masaa kumi na mbili kabla ya pambano, hakutakuwa na ruhusa ya kupunguza uzito na bondia aliyezidi uzito hataruhusiwa kupigana.

4.2.5.3. Endapo mabondia watapima uzito kwa ajili ya pambano la ubingwa wa taifa; na bingwa anayetetea ubingwa atakutwa na uzito zaidi au pungufu ya

kiwango anachotakiwa kuwa nacho na akashindwa kuupunguza au kuongeza uzito huo katika muda wa ziada kama ilivyoelekezwa hapo juu, basi bingwa huyo atapoteza ubingwa wake papo hapo kwa mtindo unaojulikana kama "*kupoteza ubingwa kwenye mizani".*

4.2.5.4. Bila ya kuathiri maelekezo ya hapo juu, pambano litaendelea kuwa la ubingwa kwa upande wa mpinzani endapo mpinzani huyo atafikisha uzito uliohitajika kwa pambano husika,

4.2.5.5. Endapo mpinzani atazidi uzito na bingwa atafikisha uzito; na bingwa akashinda pambano hilo, ubingwa bado utaendelea kushikiliwa na bingwa,

4.2.5.6. Endapo mpinzani akishinda pambano hilo, Kamisheni itamtangaza kuwa bingwa wa uzito alioupigania; na, endapo bingwa atashinda pambano hilo, Kamisheni itautangaza ubingwa huo kuwa wazi.

4.2.5.7. Endapo mabondia wote hawatafikisha kabisa uzito unaostahili kwa ajili ya pambano husika, pambano hili linaweza kuendelea kufanyika likiwa pambano lisilo la ubingwa (non title fight) na ubingwa husika utakuwa wazi,

4.2.5.8. Endapo pambano litahairishwa kwa muda usiozidi masaa arobaini na nane (48), mabondia watalazimika kupima tena uzito endapo Kamati ya Ufundi iliyo chini

ya Kamisheni itapendekeza hivyo baada ya kufanya majadiliano na wahusika

5.0. KANUNI NA TARATIBU ZA MAPAMBANO YA UBINGWA WA TAIFA NA KIMATAIFA,

Mapambano yote ya ubingwa wa Taifa na kimataifa yanayofanyika Tanzania kati ya mabondia wa Tanzania na au bondia wa nje ya Tanzania yatafanyika kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

5.1. Ubingwa wa taifa

Kamisheni ndio itakua na wajibu wa kuidhinisha kufanyika kwa mapambano ya ubingwa wa Taifa baada ya wakuzaji kuwasilisha maombi ya kuandaa mapambano ya ubingwa wa taifa.

5.2. Kamisheni itaendesha mapambano ya ubingwa wa taifa kwa nafasi za ubingwa zilizo wazi ili kutoa fursa kwa mabondia waliokidhi vigezo kushindania ubingwa wa taifa.

5.3. Bingwa wa taifa wa Tanzania katika uzito wowote atalazimika kutetea ubingwa wake kwa hiyari katika kipindi cha miezi sita (6) tangu alipotwaa ubingwa huo kwa kupambana na mmoja kati ya mabondia wanaotambuliwa katika orodha ya mabondia kumi (10) bora wa uzito wake.

5.4. Endapo bingwa atashindwa kuutetea ubingwa wake baada ya kupita miezi sita (6) Kamisheni itautangaza ubingwa huo kuwa wazi,

5.5. Bila ya kuathiri aya 5.3. hapo juu, ubingwa utakuwa wazi ikiwa mambo yafuatayo yatatokea kwa pamoja au moja kati ya hayo kwa bondia anayeshikilia ubingwa: -



TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

5.5.1. Atapewa adhabu na Kamisheni kutokana na makosa ya utovu wa nidhamu au makosa mengine yaliyoorodheshwa kwenye Kanuni za adhabu ambapo adhabu yake itakuwa ya kufungiwa kwa zaidi ya miezi kumi na mbili (12),

5.5.2. Atachezea pambano la uzito mwingine wakati akishikilia ubingwa kwa uzito husika,

5.5.3. Atashauriwa na daktari kupumzika mapambano ya ngumi za kulipwa kutokana na kuwa na matatizo ya kiafya,

5.5.4. Atapoteza pambano lolote katika kipindi ambacho atakuwa bingwa.

5.5.5. Atathibitika kutumia madawa na mbinu haramu michezoni,

5.6. Ubingwa wa kimataifa

Kamisheni pekee ndio itakua na wajibu wa kuidhinisha kufanyika kwa mapambano ya ubingwa wa kimataifa yanayofanyika Tanzania kwa kutoa idhini ya kufanyika kwa mapambano hayo baada ya muandaaji kukamilisha taratibu zote za msingi zinazohusiana na pambano la kimataifa kama ifuatavyo: -

5.6.1. Kuthibitisha mkataba kati ya muandaaji na bondia wa kimataifa angalau siku thelatihini (30) kabla ya pambano,

5.6.2. Kuwasilisha ruhusa ya kucheza nchini toka katika chombo cha kusimamia ngumi za kulipwa katika nchi anayotokea bondia siku thelathini (30) kabla ya pambano

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968.
Dar Es Salaam

5.6.3. Kuwasilisha taarifa ya afya ya bondia kwa Kamisheni siku thelathini (30) kabla ya pambano,

5.6.4. Kuwasilisha kibali cha kuendesha pambano la ubingwa kimataifa kutoka chombo kinachoendesha ubingwa huo siku thelathini kabla pambano,

5.7. Mapambano yote hayatazidi mizunguko kumi na mbili (12 rounds) kwa wanaume na mizunguko kumi (10) kwa wanawake; hayatapungua mizunguko minne (4 rounds) yenye dakika tatu (3) kwa wanaume na dakika mbili (2) kwa wanawake kwa mzunguko mmoja na mapumziko ya dakika moja (1) kati ya mzunguko mmoja na mzunguko unaofuata,

5.8. Mikataba ya kushiriki mapambano ya ngumi za kulipwa kwa mabondia.

5.8.1. Mikataba yote ya ngumi za kulipwa kati ya bondia na muandaaji itazingatia Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 ya Sheria za Tanzania pamoja vipengele vyote muhimu vya uandaaji wa mikataba ya mapambano ya ngumi za kulipwa ikiwemo: -

5.8.1.1. Kutaja waziwazi; jina la bondia anayesaini mkataba,

5.8.1.2. Jina la bondia atakayepambana naye,

5.8.1.3. Daraja la uzito watakalopigania,

5.8.1.4. Tarehe na mahali pambano litakapofanyika,

5.8.1.5. Malipo ya bondia (purse fee) kwa kushiriki pambano hilo.

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

5.8.1.6. Kwa pambano litakalofanyika ndani ya nchi, bondia wa Tanzania atakatwa asilimia mbili (2%) ya malipo ya mkataba wa pambano na fedha hizo zitatunzwa katika mfuko wa ustawi wa mabondia; bondia kutoka nje ya Tanzania atakatwa asilimia 3 (%) ya malipo ya mkataba wa pambano ambapo asilimia moja (1%) ya fedha hizo zitaingizwa katika akaunti ya mfuko wa ustawi wa mabondia na asilimia mbili (2%) zitaingizwa kwenye akaunti ya Kamisheni.

5.8.1.7. Malipo ya mabondia.

Kiwango cha chini cha malipo kwa mabondia kinapangwa kulingana na madaraja ya pambano husika kama ifuatavyo: -

Mapambano makubwa, bondia atalipwa si chini ya : -

Shilingi Laki Mbili (200,000) kwa pambano la mizunguko minne,

Shilingi Laki Tano (500,000) kwa pambao la mizunguko 6,

Shilingi Laki Nane (800,000) kwa pambano la mizunguko 8. Na,

Shilingi Milioni Tano (5,000,000) kwa pambano kuu/ubingwa.

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

Mapambano ya kati, bondia atalipwa si chini ya : -

Shilingi Laki Moja (100,000) kwa pambano la mizunguko minne,

Shilingi Laki Tatu (300,000) kwa pambao la mizunguko 6,

Shilingi Laki Tano (500,000) kwa pambano la mizunguko 8. Na,

Shilingi Milioni Moja (1,000,000) kwa pambano kuu/ubingwa.

Kamisheni itaandaa fomu mahususi ambayo itajulikana kama **“Mkataba wa pambano la ngumi za kulipwa”**

## 6.0. KANUNI NA SHERIA ZA ULINGONI

6.1. Kamisheni ya Kusimamia Ngumi za Kulipwa Tanzania inatumia Sheria Jumuishi (Unified Rules) ambazo huandaliwa na “Association of Boxing Commissions” za mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ambayo hufanyika mara kwa mara kwa mapambano yasiyo ya ubingwa. Nakala ya Sheria hizo itaambatishwa pamoja na Kanuni hizi. Wakati wote nakala ya Kingereza ndiyo itakayotumika kutoa tafsiri rasmi. Kamisheni itaanda nyaraka ya lugha ya kiswahili ya tafsiri ya Kanuni hizo kwa ajili ya matumizi kujifunzia tu.

6.2. Kwa mapambano ya ubingwa wa Kimataifa, zitatumika sheria na kanuni za vyama husika ambazo zitathibitishwa na Kamisheni kabla ya kutumika kwake.

## 7.0. WATOA HUDUMA KATIKA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA PAMOJA NA MAJUKUMU YAO

Kamisheni inatambua kwamba, watoa huduma ni kada muhimu katika kuendeleza mchezo wa ngumi za kulipwa Tanzania. Watoa huduma hawa ni; mkufunzi (coach/trainer), Msimamizi (Manager), msaidizi wa pembeni (corner man, cutman), Muandaaji (promoter), matchmaker, daktari, “ring announcer”, n.k.

Watoa huduma wote wanawajibika kwanza kuwa wanachama katika vyama shiriki kwenye kada husika ili waweze kupatiwa huduma kulingana na leseni inayotolewa na Kamisheni. Mwisho wa matumizi ya leseni ni kila ifikapo tarehe 31 Juni. Watoa huduma hao wameorodheshwa hapa chini kama ifuatavyo: -

### 7.1. Mkufunzi/kocha

Atakuwa ni mtu mwenye taaluma/uzoefu wa kutoa mafunzo ya mchezo wa ngumi za kulipwa ambaye atakuwa na jukumu la kumfundisha bondia mbinu na stadi za kupigana katika mapambano ya ngumi za kulipwa pamoja na sheria za ulingoni.

### 7.2. Msimamizi/Meneja

Meneja ni mtu binafsi au kampuni (kwa tafsiri ya sheria za makampuni na majina ya biashara za Tanzania) ambayo bondia ameingia nayo makubaliano ya kisheria ya kuwa wakala/mwakilishi wake mwenye majukumu ya kusimamia maslahi na masuala yote yanayohusiana na ukuzaji na uendelezaji wa kipaji chake pamoja na matumizi ya jina lake kama bidhaa ya kibiashara (brand). Mikataba kati ya meneja na bondia itasajiliwa pia katika Kamisheni,

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

7.3. Msaidizi wa ulingoni (corner man/cut man)

Msaidizi wa ulingoni ni msaidizi wa bondia anapokuwa ulingoni ambaye atakuwa na jukumu la kutoa huduma kwa bondia wakati wa mapambano.

7.4. Muandaaji

Ni kampuni au jina la biashara ambalo limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 na Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 ya Sheria za Tanzania ambayo moja ya kazi zake ni kuwa Muandaaji wa michezo kama anavyotambulika kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Kanuni za Usajili za Baraza la Michezo la Taifa za Mwaka 1999 na pia mwenye leseni ya Kamisheni. Wajibu wa Muandaaji ni kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa kwa: -

7.4.1. Kuingia makubaliano kati yake na mabondia pamoja na kulipa ada (purse fee) ya wachezaji

7.4.2. Kulipa ada ya kibali (sanctioning fee) kwa Kamisheni moja kwa moja kwa mapambano ya kitaifa na kimataifa. Viwango vya malipo ya vibali ni kama ifuatavyo: -

7.4.3. Pambano kubwa; Shilingi Laki Tano (500,000)

7.4.4. Pambano la kati; Shilingi Laki Mbili (200,000)

7.4.5. Pambano dogo; Shilingi Elfu Sabini (70,000)

7.4.6. Pambano la maonesho (exhibition) ambalo halitakuwa na kiingilio; bure

7.4.7. Kulipa gharama nyingine zote za uandaaji wa pambano husika ikiwemo gharama za kupima uzito na afya kwa

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968.
Dar Es Salaam

mabondia kabla na baada ya kupambana, gharama za maofisa watakaoteuliwa kuchezesha pambano husika, gharama za ulinzi wa eneo panapofanyika pambano, n.k.

7.4.8. Kulipa ada ya kibali cha pambano katika Baraza la Michezo la Taifa kiasi cha Shilingi laki moja (100,000) kwa pambano dogo na Shilingi Laki Mbili (200,000) kwa pambano kubwa.

7.5. Match Maker/wakala

Match maker ni kiunganishi kati ya bondia na Muandaaji wakati wa kuandaa pambano la ngumi za kulipwa ambaye jukumu lake ni kumtafuta bondia mwenye vigezo kwa ajili ya kushiriki pambano husika. Kwa mapambano ya Kimataifa, matchmaker/wakala atalipa asilimia moja 1% malipo yake toka kwa bondia.

7.6. Daktari (ring physician),

Mtu yeyote mwenye taaluma ya udaktari wa binadamu (doctor of medicine) na mwenye leseni ya kufanya kazi ya udaktari nchini Tanzania. Vilevile, kwa madhumuni ya Kanuni hizi, daktari pia anapaswa kuwa na ujuzi wa taaluma ya udaktari wa michezo (sports medicine) na mwanachama hai wa Chama cha Madaktari wa Tiba ya Michezo Tanzania (TASMA).

## 8.0. Utaratibu wa kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa Tanzania

Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, mapambano yote ya ngumi za kulipwa yatafanyika mara tu baada ya kupata idhini (sanction) ya Kamisheni kwa mapambano ya kitaifa na Kimataifa; Utaratibu utakaofuatwa na waandaaji wa mapambano hayo ili kupata idhini ni kama ufuatao: -

8.1. Kuwasilisha maombi ya kuandaa pambano la ngumi za kulipwa

Wakuzaji watawasilisha maombi yao kwa Kamisheni kwa maandishi katika kipindi kisichopungua siku thelathini (30) kwa mapambano ya kitaifa na siku tisini (90) kwa mapambano ya kimataifa wakibainisha yafuatayo: -

8.1.1. Kampuni/jina la biashara la Muandaaji anayeandaa pambano hilo

8.1.2. Tarehe na mahali patakapofanyika pambano hilo,

8.1.3. Orodha ya mabondia watakaocheza katika pambano hilo,

Mara baada ya maombi hayo kukubaliwa, muandaaji atapaswa kutekeleza yafuatayo: -

8.1.4. Kulipia kibali cha kuandaa pambano husika (sanctioning fee) kwa Kamisheni na kuwasilisha hati ya malipo ya benki (bank pay-in slip) angalau siku 3 tangu kupewa idhini hiyo,

8.1.5. Kuwasilisha nakala ya mikataba kati yake na mabondia wote watakaocheza siku ishirini (20) kabla ya pambano. ZINGATIA; mikataba yote ya pambano itasainiwa mbele ya mwakilishi wa Kamisheni na kushuhudiwa pia mwakilishi wa chama cha mabondia.

8.1.6. Kuweka katika akaunti ya benki ya Kamisheni malipo yote ya mabondia kwa mujibu wa mikataba, maofisa wa ulingoni na watoa huduma wengine watakaobainishwa kati yao na Muandaaji na kuwasilisha hati ya benki kwa ajili ya malipo hayo (bank pay-in slip) katika kipindi cha siku saba (7) kabla ya pambano.

8.2. Ikiwa pambano ni la kimataifa, Muandaaji anawajibika kutekeleza yafuatayo katika kipindi cha siku thelathini (30) kabla ya pambano: -

8.2.1. Kuwasilisha nakala ya ridhaa (clearence) ya bondia husika kucheza nchini kutoka katika chombo kinachosimamia ngumi za kulipwa nchini mwake, leseni amilifu ya bondia inayotolewa na chombo cha kusimamia ngumi katika taifa lake au nchi anayoishi pamoja na taarifa ya afya,

8.2.2. Kuwasilisha nakala ya mkataba wa pambano uliosainiwa na pande zote,

8.2.3. Kuwasilisha taarifa (booking) ya usafiri, malazi kwa bondia pamoja na timu yake,

Kamisheni itaitisha mkutano na waandishi wa habari ili kuuarifu umma juu ya uwepo wa pambano husika au kutoidhinisha pambano husika siku saba (7) kabla ya pambano.

Kamisheni itatoa adhabu kwa Muandaaji endapo atakiuka kipengele kimojawapo cha Ibara ya 8 hapo juu kwa mujibu wa Kanuni za Adhabu za Kamisheni.

## 9.0. UTARATIBU WA KUPANDA ULINGONI

Siku ya pambano muandaaji atawajibika kuweka mazingira rafiki kwa mabondia wanaopambana kuweza kufanya maandalizi ya mwisho kabla ya kupanda na baada ya kushuka ulingoni kwa kufanya yafuatayo: -

9.1. Mabondia watakaocheza kutokea kona ya nyekundu (red corner) watakaa tofauti na wenzao wa kona ya bluu (blue corner),

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968.
Dar Es Salaam

9.2. Bondia atapanda ulingoni akiwa na wasaidizi (seconds) wasiopunguna wawili (2) na wasiozidi wanne (4) kwa mapambano ya ubingwa na wasiozidi wawili (2) kwa mapambano yasiyo ya ubingwa ambao miongoni mwao ni lazima awepo kocha wake au cutman,

9.3. Katika mapambano yote bondia ataruhusiwa kuhudumiwa na msaidizi mmoja tu ndani ya ulingo,

9.4. Bondia atamteua na kumtambulisha kwa mwamuzi mmoja kati ya wasaidizi wake wa ulingoni kuwa “chief second” katika pambano husika kwa maamuzi ya kisheria ulingoni,

9.5. Wasaidizi wote wa ulingoni watapswa kuwa na leseni amilifu inayotolewa na Kamisheni wakati wakitimiza wajibu ulingoni,

9.6. Wasaidizi wa bondia hawataruhusiwa kuegemea ulingo, kuingia ulingoni au kuwa kwenye kona ya mpinzani wakati pambano likiendelea,

9.7. Wasaidizi wa bondia wataruhusiwa kuwa na vifaa na dawa zilizoruhusiwa kwa matumizi ya bondia wakati akiwa ulingoni baada ya vifaa na dawa hizo kukaguliwa na kuthibitishwa na msimamizi (supervisor) wa mchezo husika.

9.8. Mwamuzi ndio atakuwa na maamuzi ya mwisho (sole arbitor) katika pambano husika ulingoni. Sheria hii haitazuia ukaguzi wa video au ukaguzi mwingine wa uamuzi uliofanywa na mwamuzi ulingoni chini ya taratibu za mamlaka ya udhibiti inayotumika ikiwa malalamiko yatawasilishwa kwa madai ya ukiukaji wa wazi wa kanuni.

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968,
Dar Es Salaam

9.9. Endapo afisa yeyote wa ulingoni akiwa katika kutimiza majukumu yake ataharibu pambano kwa makusudi atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufungiwa au kupigwa faini au vyote viwili

## 10.0. UTARATIBU WA KUSAFIRI NJE YA NCHI KWA AJILI YA MAPAMBANO YA NGUMI ZA KULIPWA

Katika kuhakikisha ubora wa viwango na uwezo kiushindani wa bondia pamoja na kulinda maslahi ya bondia. Kocha/Msimamizi/wakala wa bondia atawajibika kutoa taarifa kwa Kamisheni angalau siku siku ishirini (20) kabla ya safari. Taarifa hiyo ataambatisha pamoja na: -

10.1. Mkataba halisi (original copy of the contract) wa pambano husika pamoja na barua za mwaliko,

10.2. Nakala ya hati za kusafiria kwa wote watakaoambatana na bondia katika safari hiyo,

10.3. Kamisheni ikiridhia maombi hayo itawasilisha maombi ya kibali cha kusafiri nje ya nchi katika Baraza la Michezo la Taifa kama kinavyoelekeza Kifungu cha 17 (1) na (4) cha Kanuni za Baraza la Michezo la Taifa za Mwaka 1999,

10.4. Bondoa atalipia katika akaunti ya Kamisheni asilimia tano (5%) ya malipo hayo kama yalivyooneshwa kwenye mkataba wa pambano husika ambapo Kamisheni itaweka asilimia moja (1%) katika akaunti ya Chama cha Mabondia.

10.5. Kamisheni itaandika barua ya kumruhusu bondia (clearence letter) kwa chombo cha kusimamia ngumi za kulipwa katika nchi ambayo bondia atakwenda kupigana,

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968
Dar Es Salaam

10.6. Timu ya bondia itawasilisha katika Kamati ya Ufundi ya Kamisheni programu ya maandalizi ya bondia husika ili kufanya tathmini na kutoa ushauri wa namna bora kujiandaa.

10.7. Kima cha chini cha malipo kwa mabondia kwa mapambano ya nje ya nchi: -

Kiwango cha chini cha malipo kwa mabondia kulingana na viwango vyao kitakuwa kama ifuatavyo: -

10.7.1. Nyota moja hadi moja na nusu – USD 3000/=

10.7.2. Nyota moja na nusu – USD 5000/=

10.7.3. Nyota mbili hadi mbili na nusu – USD 8000/=

10.7.4. Nyota tatu – USD 12000/=

10.7.5. Nyota nne – USD 25000/=

10.7.6. Nyota tano – USD 50000/=

TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION
TPBRC
P.O. Box No. 9968.
Dar Es Salaam

| | |
|---|---|
| Jina na saini | Jina na saini |
| Chaurembo Palasa | Yahya Poli |
| Rais | Katibu |

VIMBATISHO

Viambatisho ambavyo vitasomwa na Kanuni hizi ni nyaraka mahususi ambazo zitatoa maelekezo juu ya masuala mbalimbali ambayo yametajwa katika Kanuni hizi kama ifuatavyo: -

10.8. Kiambatisho I – Association of Boxing Commissions; Unified Rules of Boxing[1]

10.9. Kiambatisho II – Jedwali la ada mbalimbali zinazolipwa katika Kamisheni

10.10. Kiambatisho III – mkataba wa pambano (Fomu Na. 1)

10.11. Kiambatisho IV – Fomu ya maombi ya leseni kwa Muandaaji (Fomu Na. 2)

10.12. Kiambatisho V – Fomu ya Maombi ya leseni kwa bondia, n.k. (Fomu Na. 3)

10.13. Kiambatisho VI – Bout Agreement (Form No. 4)

[1] http://www.abcboxing.com/wp-content/uploads/2016/10/unified_rules_boxing_rev_august2016.pdf

## ASSOCIATION OF BOXING COMMISSIONS (ABC)

### <u>SHERIA JUMUISHI ZA NGUMI</u>

***(kama zilivyothibitishwa Agosti 25, 2001. Marekebisho ya Agosti 2, 2002, Marekebisho ya Julai 24, 2012, Marekebisho ya Julai 29, 2014, Marekebisho ya Agosti 3, 2016).***

1. Kila mzunguko utakuwa na dakika tatu (3) za mchezo na dakika moja (1) ya mapumziko kati ya mzunguko mmoja na mzunguko mwingine

2. Mwamuzi wa pambano ndiye mtu pekee aliyeidhinishwa kusitisha pambano. Sheria hii haitazuia ukaguzi wa video au ukaguzi mwingine wa uamuzi uliofanywa na mwamuzi ulingoni chini ya taratibu za mamlaka ya udhibiti inayotumika ikiwa malalamiko yatawasilishwa kwa madai ya ukiukaji wa wazi wa kanuni.

3. Mapambano yote yataamuliwa kwa uamuzi wa majaji watatu (3).

4. Mfumo wa alama 10 ndio utakaotumika na majaji watatu katika kufanya maamuzi.

5. Mfumo wa kuhesabu mpaka Nane (8) baada ya “knockdown” ndio utakaotumika katika mapambano yote.

6. Mabondia wote wa kulipwa wanawajibika kuvaa kikinga kinywa wanapokuwa ulingoni. Mzunguko hauwezi kuanza ikiwa bondia hajavaa kikinga kinywa. Ikiwa kikinga kinywa kitadondoka wakati pambano likiendelea, mwamuzi atasimamisha pambano na kuhakikisha bondia anavalishwa kikinga kinywa haraka iwekanavyo. Bondia anaweza kupunguziwa alama ikiwa ataona kwamba bondia ametema kikinga kinywa kwa makusudi.

7. Hakutakuwa na kuhesabiwa kwa nukta Nane (8) ikiwa bondia amesimama.

8. Sheria ya "Knockdown" tatu (3) haitatumika.

9. Bondia atahesabiwa nukta ishirini (20) ikiwa atatolewa nje ya ulingo kwa konde. Bondia hapaswi kusaidiwa na watazamaji au wasaidizi wake wa ulingoni. Iwapo atasaidiwa na mtu yeyote, bondia huyo anaweza kupoteza pointi au kuenguliwa huku uamuzi huo ukiwa ndani ya uamuzi wa mwamuzi pekee.

10. Bondia ambaye amedondoshwa hatookolewa na kengele katika mzunguko wowote ule.

11. Ikiwa bondia atapata jeraha litokanalo na konde halali na ikiwa jeraha hilo ni kubwa kiasi cha kukatisha pambano, bondia aliyejeruhiwa atapoteza pambano kwa TKO.

12. Majeraha yatokanayo na faulo:

**A. Faulo za makusudi**

1. Ikiwa faulo ya makusudi itasababisha jeraha na ikiwa jeraha hilo ni kubwa kiasi cha kusababisha kukatisha pambano mara moja. Bondia aliyesababisha jeraha atapoteza kwa "disqualification".

2. Ikiwa faulo ya makusudi itasababisha jeraha nab ado pambano likaendelea, mwamuzi ataitaarifu mamlaka na kukata alama mbili (2) kutoka kwa bondia aliyesababisha jeraha hilo. Kukatwa alama kwa faulo za makusudi ni lazima.

3. Ikiwa faulo ya makusudi itasababisha jeraha na pambano bado likaruhusiwa kuendelea, na jeraha hilo likasababisha pambano kutoendelea baada ya mzunguko wa Nne (4), bondia aliyejeruhiwa atashinda kwa "TECHNICAL DECISION" ikiwa yeye ndiye atakayekuwa anaongoza kwa alama; na pambano litakuwa "TECHNICAL DRAW" ikiwa bondia aliyejeruhiwa atakuwa nyuma kwa alama au watakuwa na alama sawa.

4. Ikiwa bondia atajijeruhi mwenyewe wakati akijaribu kufanya faulo kwa mpinzani wake kwa makusudi, mwamuzi hatochukua hatua yoyote kwa ajili yake, na jeraha hili litahesabika kama amepigwa konde halali.

5. Ikiwa mwamuzi ataona kwamba bondia anaonesha tabia zisizo za kiuanamichezo, anaweza kusitisha pambano na kuamua kwa mtindo wa "disqualification" kwa bondia aliyeonesha tabia hizo.

**B. Faulo zisizo za makusudi**

1. Ikiwa faulo isiyo ya makusudi itasababisha jeraha kubwa ambalo litatosha kwa kumfanya mwamuzi asimamishe pambano, pambano hilo litaamuliwa kwa mtindo wa "NO CONTEST" ikiwa pambano hilo litasimamishwa kabla ya kukamilika kwa mizunguko minne (4). Mizunguko mine (4) inakamilika pale tu kengele inapogongwa kuashiria nwisho wa mzunguko wan nne.

2. Ikiwa ajali isiyo ya makusudi itasababisha jeraha kiasi cha kutosha kwa mwamuzi kusimamisha pambano baada ya mizunguko minne kufanyika, pambano litaamuliwa kwa "TECHNICAL DECISION" kwa bondia ambaye atakuwa anaongoza kwa alama wakati pambano hilo linasimamishwa.
    a. Mzunguko ambao haujakamilika utaamuliwa. Ikiwa hakuna tendo litakalotokea, mzunguko huo utaamuliwa sawa. Hii ni kwa hiari ya majaji.

13. Bondia atakayepigwa chini ya mkanda bila ya kukusudia ni lazima aendelee na pambano baada ya kupewa muda wa kupumzika usiozidi dakika tano (5), vinginevyo atapoteza pambano .

JEDWALI LA ADA NA TOZO MB ALIMBALI ZINAZOLIPWA KATIKA KAMISHENI (TPBRC) PAMOJA NA BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

| NA. | ADA/TOZO | MALIPO (TZS) NA TAASISI INAYOLIPWA | | MUDA WA KULIPA |
|---|---|---|---|---|
| | | TPBRC | BMT | |
| 1. | Kibali cha pambano dogo | 70,000 | 100,000 | Siku 14 kabla ya pambano |
| 2. | Kibali cha pambano la kati | 100,000 | 100,000 | Siku 14 kabla ya pambano |
| 3. | Kibali cha pambano kubwa | 500,000 | 200,000 | Siku 14 kabla ya pambano |
| 4. | Kibali cha bondia kupigana nje ya nchi | Asilimia tano (5%) ya malipo kwa mujibu wa mkataba | 50,000 | Siku 14 kabla ya safari/pambano |
| 5. | Kibali cha bondia kutoka nje kupigana Tanzania | Asilimia tatu (3%) ya malipo kwa mujibu wa mkataba | 2000,000 | Siku 14 kabla ya pambano |
| 6. | Leseni ya mkuzaji | 50,000 | | Leseni kwa kada zote mwisho wake wa matumizi ni tarehe 31 Juni. |
| 7. | Leseni ya msimamizi wa bondia | 50,000 | | |
| 8. | Leseni ya wakala na matchmaker | 50,000 | | |
| 9. | Leseni ya bondia | 12,000 | | |
| 10. | Leseni ya "card girl" | 25,000 | | |
| 11. | Leseni ya "ring announcer" | 50,000 | | |
| 12. | Leseni ya kocha/msaidizi wa ulingoni | 20,000 | | |
| 13. | Leseni ya "ring physician" | 50,000 | | |

**FOMU NA. 01**

**MKATABA KATI YA BONDIA NA MKUZAJI**
**MAHUSUSI KWA AJILI YA PAMBANO LA NGUMI ZA KULIPWA**

**Mkataba huu umefungwa leo tarehe ______ mwezi _________________ mwaka _____________**

**KATI YA**

**________________________________________** S.L.P ___________, ________________________, Namba ya Usajili/Cheti _________________ (BRELA), ______________ (BMT); Namba ya Leseni ___________ (TPBRC)**,** ambaye kwenye mkataba huu atajulikana kama "**Mkuzaji**" kwa upande mmoja,

**NA**

**_______________________________,** Simu______________, ____________________, ambaye amesajiliwa kama "bondia wa kulipwa" na kupewa Leseni Namba ________________ ambaye kwenye mkataba huu atajulikana kama "**BONDIA**" kwa upande mwingine,

**KATIKA MKATABA HUU, WAHUSIKA WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO: -**

1. Kwamba, bondia anakubali kwa hiari yake, kushiriki katika pambano la ngumi za kulipwa dhidi ya ______________________________________ katika uzito wa ________Kg, mizunguko _________ Ubingwa wa ______________________________________/lisilo la ubingwa litakalofanyika (taja tarehe na mahali/mji) _____________________________________________________________________________.

2. Kwamba, ikiwa mpinzani atabadilishwa, mkuzaji atapaswa kumtaarifu bondia angalau masaa 72 (siku 3) kabla ya siku ya pambano mara baada ya mpinzani huyo kuthibitishwa na Kamisheni.

3. Kwamba, Bondia atawajibika kufanya vipimo vya afya ikiwemo Hepatitis B & C, HIV na Syphillis na atapima uzito baada ya kutaarifiwa na Mkuzaji siku, muda na mahali ambapo zoezi la kupima afya na uzito litafanyika.

4. Kwamba, ikiwa pambano litafanyika katika mji anaoishi bondia, Bondia na timu yake watajigharimia usafiri na wanawajibika kufika eneo la tukio saa moja kabla ya kuanza ratiba ya kupima uzito.

5. Kwamba, endapo bondia atafika wakati zoezi la kupima uzito limeshaanza, atakatwa asilimia mbili (2%) ya pesa yake ya malipo kwa pambano hilo. Endapo zoezi la kupima uzito litachelewa kuanza kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Mkuzaji, Mkuzaji atawajibika kumlipa bondia asilimia 2 ya ziada katika pesa ya malipo ya bondia kwa mujibu wa makubaliano.

6. Kwamba, endapo bondia atazidi uzito kinyume na uzito uliotajwa hapo juu, atapewa masaa mawili ya kupunguza ili kufikia kiwango cha uzito kwa mujibu wa makubaliano. Ikiwa bondia atashindwa kupunguza uzito baada ya masaa mawili na kwa makubaliano kati yake, mpinzani wake na Kamisheni watakubaliana kuendelea na pambano, bondia atawajibika kumlipa mpinzani wake kiasi cha asilimia ______________ kutoka katika pesa yake ya malipo kwa ajili ya pambano hilo.

7. Kwamba, bondia anawajibika kucheza kwa kiwango na ustadi wa hali ya juu na endapo atacheza chini ya kiwango na Kamishna wa pambano hilo akajiridhisha kwamba bondia amecheza chini ya kiwango ama hakuwa tayari kucheza Kamisheni itazuia malipo yake yote au itakata sehemu ya malipo hayo.

8. Kwamba, bondia anafahamu kuwa mchezo wa ngumi za kulipwa unaweza kuhatarisha maisha/afya yake na yuko tayari kuendelea kushiriki na kwamba Mkuzaji hatowajibika kwa madhara ambayo bondia atayapata ulingoni.

9. Kwamba, Mkuzaji atamlipa Bondia kiasi cha __________________________________________ kama malipo halali ya pambano hilo mara tu baada ya kushuka ulingoni siku ya pambano. Bondia atakatwa asilimia mbili (2%) ya malipo yake kwa ajili ya mfuko waTPBRC. Endapo kutakuwa na makato yoyote mengine katika malipo hayo, makato hayo yatafanyika kabla ya bondia kukabidhiwa pesa yake.

10. Kwamba, mara baada ya kusaini mkataba huu, Bondia hatoruhusiwa kushiriki pambano lolote katika kipindi cha siku ______________ kabla ya pambano hilo na muda wote huo atapaswa kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya pambano hilo.

11. Kwamba, Bondia atawajibika kutoa ushirikiano kwa Mkuzaji wakati wote wa maandalizi ya pambano hilo ikiwemo kushiriki kikamilifu katika mikutano na waandishi wa habari, kurekodi matangazo ya pambano kwa ajili ya redio, video na mitandao ya kijamii. Mkuzaji atawajibika kulipia gharama ya usafiri na chakula kwa bondia wakati wote atakapomtumia bondia kwa ajili ya kutangaza pambano hilo kwa kadri ya makubaliano yao.

12. Kwamba, Mkuzaji atawajibika kugharamia usafiri, chakula, malazi kwa watu _____________ akiwemo bondia mwenyewe ikiwa pambano linafanyika nje ya mji anaoishi bondi.

13. Kwamba, bondia na timu yake watajigharamia usafiri na watafika katika ukumbi/mahali panapofanyikia pambano masaa mawili kabla ya ratiba ya mapambano kuanza na bondia atapaswa kuwa tayari kupanda ulingoni mara baada ya kuitwa na mtangazaji kwa ajili hiyo.

14. Kwamba, iwapo Bondia atakiuka mojawapo ya masharti ya mkataba huu atawajibika kumlipa Mkuzaji gharama zake zinazohusiana na maandalizi ya pambano hilo kwa Bondia ikiwemo matangazo ya vipeperushi, redio, runinga na mitandao ya kijamii, mikutano na waandishi wa habari pamoja na gharama nyinginezo za halali na zitakazothibitishwa.

15. Kwamba, iwapo Mkuzaji atavunja au atahairisha pambano kutokana na majanga ya asili, atawajibika kupanga tarehe nyingine ya pambano na Bondia hatomdai fidia Mkuzaji itokanayo na kuvunjika au kuhairishwa kwa pambano hilo.

16. Kwamba, iwapo Mkuzaji atavunja au kuhairisha pambano kwa sababu nyingine yoyote isiyokuwa ya majanga ya asili atawajibika kumlipa fidia bondia asilimia ____________ (________%) ya malipo ambayo angelipwa bondia kama ilivyooneshwa katika aya ya 6 hapo juu.

17. Kwamba, makubaliano mengine yoyote yatokanayo na au nje ya mkataba huu, yatapswa kuwa katika maandishi na kukubaliwa na pande zote zilizoweka saini zao kwenye mkataba huu, hususan Bondia na Mkuzaji.

18. Kwa kuweka saini zao, Mkuzaji na Bondia wanakubaliana kwamba makubaliano haya ni halali na yatalindwa na sheria za Tanzania.

**KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA**, wahusika wa mkataba huu wanasaini mkataba huu kama ifuatavyo;

**Mkuzaji**
Jina: ___________________________________
Saini: __________________________________
Anuani Ya Posta: ________________________
Wadhifa: _______________________________
Tarehe: ________________________________

Muhuri

**Bondia**
Jina: ___________________________________
Saini: __________________________________
Tarehe: ________________________________

**Kocha/Meneja**
Jina: ___________________________________
Saini: __________________________________
Tarehe: ________________________________

**MAKUBALIANO HAYA YAMETHIBITISHWA NA KAMISHENI YA KUSIMAMIA NGUMI ZA KULIPWA TANZANIA**

Jina: ___________________________________
Saini: __________________________________
Anuani Ya Posta: ________________________
Wadhifa: _______________________________
Tarehe: ________________________________

**Form No. 2**

**BOUT CONTRACT**

This contract is made this _________ day of _____________________, 201__

**BY AND BETWEEN**

_________________________________________ of P. O. Box _________, ___________________ duly registered promotion firm under the laws of the United Republic of Tanzania and Licensed to Promote Professional Boxing by the Tanzania Professional Boxing Regulatory Commission (TPBRC) with valid License No. _________ hereinafter to be referred to as "Promoter" on the one part.

**AND**

____________________________ of ____________________________________ a duly licensed Professional Boxer with Valid License No. ________ issued by ___________________________hereinafterto be referred to as "Boxer" on the other part.

**WHEREAS,** the Promoter undertakes to arrange and the Boxer undertake to participate in the underwritten boxing bout, hereinafter referred to as 'Bout', contesting for the non-title/title _________________________________________Title, weigh-in ____________ Kg, _________ rounds against _________________________________

**NOW THIS CONTRACT WITNESSETH AS FOLLOWS: -**

1. That, the Boxer shall arrive in the bout city not later than _________________________, 20____.

2. That, the Boxer shall undergo the official Weigh-ins procedure for the bout which shall take place on ____________________________ at ________ o'clock in the city of __________________________________________.

3. That, the Boxer shall submit a copy of authorization letter to box from the Boxing Commission of his country not later than _______ days before the date of fight.

4. That, the weight as well as the brand and model of the boxing gloves shall be supplied by the Promoter and approved by the Commission. The parties herein agree that in no circumstances the boxing gloves weight shall be contrary to weight specified as ____ ounces.

5. That, the boxer MUST send to Promoter through email all of his current (taken not later than ______days) medical documents/results including MRI and MRA Head results, Ophthalmologic Exam results, Hepatitis B & C exam reports, Antigen result, HIV/AIDS test results, Chest X-Ray results, Electro Encephalogram and Electro Cardiogram not later than ten (10) days before the bout. The Commission shall direct the boxer to undergo the above mentioned medical examinations before allowing the bout to take place.

6. That, prior to the bout, the boxer shall submit to the Tanzania Professional Boxing Regulatory Commission (the Commission) and Promoter a valid Boxer's License and a bout participation permit (Authorization Letter) issued by the __________________________________

7. That, the Promoter shall pay unto the Boxer, and the Boxer shall accept a purse in the amount of ____________________________________ (_______________/=) only. Three percent (3%) of the said boxer's purse money shall be deducted for the Commission's fund and after the deduction the purse should be effected immediately after the conclusion of the bout directly to the Boxer or his designated person.

8. That, in case the Boxer refuses to participate in the bout, the Boxer shall be liable to pay unto the Promoter 40% of the purse specified in paragraph 8 of the present contract.

9. That, the promoter shall provide for economy class round-trip _____________ to the Boxer and his ________________. The Boxer and his team shall assume responsibility to obtain visa and other related travel documents.

10. That, the Promoter shall be liable to provide the Boxer and his team with accommodation (hotel), intra-town transport and meals during their stay in ___________________

11. That, the Boxer shall participate in all events arranged by the Promoter and targeted at promotion and assistance to the bout including but not limited to; press conference, demo trainings, public appearance, e.t.c. The list and time-table to such events shall be presented to the Boxer by the Promoter at the arrival date.

12. That, it is understood and agreed that the rights and obligations of the parties hereto shall be governed by, and construed according to the laws of the United Republic of Tanzania. The terms of this agreement shall, in all respects, be in conformity with the laws of the United Republic of Tanzania as well as the rules and regulations now, or hereafter, adopted by the Commission.

13. The Boxer understands by participating in a contest or exhibition of boxing, that the Boxer is engaging in an abnormally dangerous activity. The Boxer further understands that this participation subjects the Boxer to a risk of severe injury or death. The Boxer, with full knowledge of this risk, nonetheless, agrees to enter into this agreement and hereby waives any claim that the Boxer or Boxer's heirs may have against the Promoter and/or the Commission

as the result of any injury the Boxer may suffer as a result of Boxer's participation in any contest or exhibition of boxing.

14. The parties, jointly and severally hereby indemnify and hold harmless the Promoter and the Commission, and each of their members, agents, and employees in their individual, personal and representative capacities against any and all claims, suits and actions, brought against the persons named in this paragraph by reason of this agreement and all other matters relating thereto, and against any and all expenses, damages, charges and costs, including court costs and attorney fees which may be incurred by the persons and entities named in this paragraph as a result of said claims, suits and actions.

15. That, if any party herein breaches this contract, the non-breaching party shall have all remedies available at law or in equity.

16. That, the Promoter and the Boxer agree to fulfill, in good faith, the terms and conditions of this contract during the period covered by this contract. It is understood and agreed that if the Boxer enters into another contest within 20 days prior to this bout and lessens his/her value, the Promoter shall have the option of modifying or canceling this contract.

17. That. the promoter is responsible for and shall make all the necessary arrangements in accordance with Laws of United Republic of Tanzania and Tanzania Professional Boxing Commission rules/regulations for said contest

**OTHER ITEMS** agreed to by Boxer and Promoter include: -

I. This contract shall be submitted to and approved by the Commission before weigh-ins.

II. No modification or amendment to this contract shall be binding upon the parties unless the same is in writing, signed by the respective parties hereto, and filed with and approved by the Commission.

**PARTIES SIGNATURE**

**PROMOTER:**
Name of the Official: ___________________________
Signature: ___________________________________
Postal Address: ________________________________ official seal/stamp
Occupation: __________________________________
Date: _________________________________________

**BOXER**:
Signature: ___________________________________
Date: _________________________________________

**MANAGER** or **AUTHORIZED PERSON BY THE BOXER**
Name: ________________________________________
Signature: ___________________________________
Date: _________________________________________

**COMMISSION APPROVAL:**
Name of the Official: ___________________________
Signature: ___________________________________
Postal Address: ________________________________ official seal/stamp
Occupation: __________________________________
Date: _________________________________________

Fomu Na. 3

Weka picha ya passport size ya rangi hapa

## FOMU YA MAOMBI YA LESENI

**1.0. TAARIFA BINAFSI ZA MWOMBAJI**

1.1. Jina la la mwombaji (andika majina matatu) ________________________________

1.2. Jina la ulingoni (ring name)____________________________________________

1.3. Tarehe ya kuzaliwa: ________ mwezi: ___________________, mwaka: __________

1.4. Anuani ya makazi: namba ya nyumba: _____________ mtaa: __________________________
kata: _________________________ wilaya: _______________________________________
mkoa: ______________________________ namba ya Simu: __________________________
barua pepe: ____________________________________________________________________

1.5. Jinsia: M'ke [ ] M'me [ ] urefu/kimo ____________. Urefu wa mikono ___________________

1.6. Namba ya utambulisho Boxrec: _________________

1.7. Aina ya kitambulisho:-

a) Hati ya kusafiria [ ] Namba: _______________________
b) Kitambulisho cha uraia [ ] Namba: __________________
c) Kadi ya mpiga kura [ ] Namba: _____________________
d) Kingine (taja) _____________________________________

**2.0. TAARIFA KUHUSU LESENI**

2.1. Aina ya leseni inayoombwa. Weka alama ya tiki [√] kwenye eneo unaloomba.
Bondia [ ], Kocha [ ], Mwamuzi [ ], Ofisa wa ulingoni [ ], Daktari [ ],
Msaidizi wa ulingoni [ ], Meneja [ ].

Kama mwombaji ni bondia na uko chini ya usimamizi wa meneja, taja jina la meneja wako ________________________________________

Kama mwombaji ni msimamizi wa bondia, taja jina/majina ya mabondia unaowasimamia na ambatisha na nakala mikataba ya usimamizi: ___________________________________________

Mimi _________________________ ambaye ni mwombaji wa leseni tajwa hapo juu, ninakiri na kuthibitisha kwamba, taarifa nilizozitoa hapa ni za kweli.

Saini ya mwombaji ___________________________ tarehe ____________________________________________

**KWA MATUMIZ YA OFISI:**
Namba ya Leseni: __________________
Tarehe ya kuidhinishwa na kuanza kutumika: __________________ tarehe ya ukomo: _____________________
Jina na saini ya Rais: __________________________________________

Fomu Na. 4

## FOMU YA MAOMBI YA LESENI

3.0. TAARIFA ZA MWOMBAJI

3.1. Jina la mwombaji (andika jina la Kampuni au jina la biashara)/company or business name:

........................................................................................................................................

3.2. Namba ya cheti cha usajili(BRELA)/Certificate No. .............................................................

3.3. Namba ya usajili Baraza la Michezo/Registration No. National Sports Council .....................

3.4. Anuani/physical address: namba ya nyumba/House No: ..................... mtaa/street: ............................... kata/ward:........................................ wilaya/district: ............................., mkoa/region:............................... Namba ya Simu/mobile:............................................. barua pepe/email: ......................................................

3.5. Namba ya utambulisho Boxrec/Boxrec Identification No: ....................................

4.0. TAARIFA KUHUSU LESENI/CATEGORY OF LICENSE APPLIED FOR:

4.1. Aina ya leseni inayoombwa/Licence category: .......................................................

Mimi/I ...................................................... ambaye ni/being the ................................ wa/of ........................................................ ambaye ni mwombaji wa leseni tajwa hapo juu, ninakiri na kuthibitisha kwamba, taarifa nilizozitoa hapa ni za kweli/ applicant of the above mentioned licence declare that all the information I provided above are true.

Saini na muhuri/signature and stamp ...................................... jina/name ..........................................

Cheo/title ............................................. tarehe/date ................................................

KWA MATUMIZI YA OFISI/FOR OFFICIAL USE:

Namba ya Leseni/licence number: ...............................................

Tarehe ya kuidhinishwa na kuanza kutumika/date issued: ........... tarehe ya ukomo/expiry date : .............

Jina na saini ya ofisa aliyetoa leseni/Name and signature of the officer issuing the licence:

............................................................................. tarehe/date ......................................................